- nusa	smell
- shika	touch, hold
- sema	talk, speak, say
-tafuna	chew

EXPRESSIONS

Kupata nafuu	to get well
Ninasikia maumivu, uchungu	I'm having pains

GRAMMAR EXPLANATION:
THE PASSIVE VERBS:
In this unit, we find constructions like:

Ninaumwa na	-	***I am being pained by***
Utapimwa	-	***You will be examined***
Utapelekwa	-	***You will be taken***

Constructions of these kinds are called **Passive Constructions.**

1. Verbs of Bantu origin that end in 'a' are changed into passive by the addition of infix -w- just before the final vowel - "A" of the verb.

Examples:

Active	**Passive**	**Meaning**
Kuuma	Kuuma	to be pained
Kupeleka	Kupelekwa	to be taken
Kuandika	Kuandikwa	to be written
Kupika	Kupikwa	to be cooked
Kukata	Kukatwa	to be cut

Chakula kilipikwa na mama ***The food was cooked by mother***

2. The verbs that end in double vowels "OA" in the passive form, the final -A- is replaced by "LEWA" for example

Active	**Passive**	**Meaning**
Kuoa	Kuolewa	to be married
Kuondoa	Kuondolewa	to be removed
Kutoa	Kutolewa	to be taken out
Kungoa	Kungolewa	to be uprooted

Nilingolewa jino na daktari - ***My tooth was uprooted by the doctor***

3. VERBS ENDING IN "UA" or "AA". Here in the passive the final -A- is replaced by "LIWA". For example.

Active	**Passive**	**Meaning**
Kuua	Kuuliwa	to be killed
Kununua	Kununuliwa	to be bought
Kuzaa	Kuzaliwa	to be born

Hosted for free on livelingua.com

Kukaa	Kukaliwa	to be sat on
Chakula kilinunuliwa na mkubwa	***The food was bought by the boss.***	

4. VERBS ENDING IN 'I' OR 'E'

For all the verbs in this category -**"WA" i**s suffixed Examples.

Active	**Passive**	**English**
Kutaliki	Kutalikiwa	(to be divorced)
Kufasiri	Kufasiriwa	(to be translated)
Kusamehe	Kusamehewa	(to be forgiven)

5. VERBS ENDING IN "U" PROCEDED BY A CONSONANT.

In this case the Final "U" is replaced by "IWA" Examples:

Active	**Passive**	**English**
Kuhukumu	Kuhukumiwa	(to be judged)
Kujibu	Kujibiwa	(to be answered)
Kajaribu	Kujaribiwa	(to be tried)
Kuhesabu	Kuhesabiwa	(to be counted)

Note:

Monosyllabic Verbs have each their own version.

e.g. Kula changes to kuliwa - ***to be eaten***

Kunywa changes to kunywewa - ***to be drunk (not intoxicated)***

Note: Usually passive verbs are followed by a conjunction such as "by" or 'with', i.e.

Mtoto alikatwa kwa kisu - ***The child was cut with a knife.***

Chakula kilipikwa na mpishi - ***The food was cooked by the Chef***

If the conjunction refers to human, the word used is 'na' and if it refers to things, then the word used is 'kwa'.



ZOEZI 1- EXERCISE 1

Tafsiri sentensi hizi - Translate these sentenses

1. If people eat vegetables and fruits, they will be healthy.

2. If people feel cold, they can get colds.

3. You need to boil drinking water inorder to prevent water borne diseases.

Hosted for free on livelingua.com

4. If you have diarrhea you must drink a lot of water.

5. If your joints are aching you need to see a doctor.

6. Joe has lost appetite.

7. That patient should eat alot of fruits.

8. If people don't use their toilets well they'll get many diseases.

9. If you drink dirty water, you'll get typhoid.

10. If you don't wash your hands before eating you will have stomachache.


EXERCISE I1 - ZOEZI II

Write the passives of the following sentenses:


1. Otieno alimpiga Kimani.....
2. Nyoka alimwuma mtoto wa jirani.....
3. Mama amepeleka mtoto hospitali.....
4. Wapishi walipika chakula kingi.....
5. Alice alisafisha chumba cha wageni.....
6. Ken alijibu maswali yote.....
7. Mkubwa alimsamehe askari aliyeiba.....
8. Hakimu alimhukumu mwizi yule.....
9. Walimu waliandika ki kipya.....
10. Mzungu alinunua chaku ote.....

EXERCISE III - ZOEZ

Name the following parts of the Body. Ar ya viungo vya mwili vifuatavyo



Hosted for free on livelingua.com



EXERCISE IV - ZOEZI IV

Maliza Sentensi zifuatazo ukitumia viungo vya mwili (Complete the following sentences using parts of the body)

1. Tunaona Kwa _____
2. Tunasikia kwa _____
3. Tunatembea kwa _____
4. Tunakaa kwa _____
5. Tunashika kwa _____
6. Tunakula kwa _____
7. Tunatafuna kwa_____
8. Tunanusa kwa _____
9. Tunaandika kwa _____
10. Tunabeba mizigo kwa _____

Cultural Note

- Inquiring about each other shealth and expressing sympathy for one another important aspects of social interactions.

Hosted for free on livelingua.com

- People frequently visit their sick friends, relatives workmates or neighbours to give needed support, or help, and wish them quick recovery.
- People are usually visited alot and are always with people when they are sick, hence it'll be hard to convince them to leave you alone, for personal space.
- It's appreciated if you give money or food to sick friends.
- Being big / heavy is a sign of wealth and health.
- In some societies, when someone dies from certain diseases, people believe that they have been bewitched.

LESSON 15

TOPIC: DIRECTIONS

COMPETENCY: ASK, GIVE AND FOLLOW DIRECTIONS

MAZUNGUMZO 1 - DIALOGUE 1

Lusimba:	Habari yako?	***How are you?***
Ezekiel:	Salama sana. Naweweje?	***Very well, and you?***
Lusimba:	Fiti sana.	***Very well.***
Ezekiel:	NInaweza kukusaidia?	***Can I help you?***
Lusimba:	Ndiyo	***Yes.***
Ezekiel:	Unashida gani?	***What problem do you have?***
Lusimba:	Mimi ni mgeni hapa Naivasha na ninataka kwenda posta. Tafadhali nionyeshe njia.	***I am a visitor here in Naivasha and I want to go to the Post Office. Please show me the way.***
Ezekiel:	Fuata hii barabara ya biashara. Hapo mbele kidogo, utaona makutano ya barabara. Pinda kulia halafu nenda moja kwa moja. Mbele kidogo, utaona Posta iko karibu na	***Follow this biashara street, a little bit** infront **of you, you will see the road junction. Turn right then go straight. Infront you will see the Post Office. It is near the Barclays Bank.***

Hosted for free on livelingua.com

	Benki ya Barclays.	
Lusimba:	Ni mbali sana?	***Is it very far?***
Ezekiel:	Hapana ni karibu sana. Kutembea ni kama dakika tano tu.	***No it's very near. It is about five minutes walk.***
Lusimba:	Asante sana.	***Thank very much***
Ezekiel:	Karibu	***Welcome***

MAZUNGUMZO 2 - DIALOGUE 2

Ezekiel:	Habari za asubuhi Bwana Moses	***Good morning Mr. Moses.***
Moses:	Salama.	***Fine***
Ezekiel:	Mwanafunzi Tina yuko wapi?	***Where is Tine the student?***
Moses:	Yuko darasani.	***She is in class***
Ezekiel:	Jana alikuwa wapi?	***Where was she yesterday?***
Moses:	Alikuwa nyumbani.	***She was at home.***
Ezekiel:	Kwa nini hakuja darasani jana?	***Why did she not come to class yesterday?***
Moses:	Anasema alikuwa mgonjwa.	***She says she was sick.***
Ezekiel:	Sasa anaendeleaje na masomo?	***How is she doing in lessons.***
Moses:	Vizuri tu.	***Very well***
Ezekiel:	Haya asante kwa habari.	***Thanks for the news***
Moses:	Asante kwaheri.	***Thanks and goodbye.***

MSAMIATI - VOCABULARY

PREPOSITIONS:

Kiswahili	**English Equivalent**
karibu na	Near
mbele ya	Infornt of
nyuma ya	behind
nje ya	out of / outside of
ndani ya	in/inside of
mbali na	Far from
baina ya	Between / in between / among
kati ya / katikati ya	in the middle of

Hosted for free on livelingua.com

VERBS:

Kiswahili	**English Equivalent**
nionyeshe	show me
fuata	follow
pinda	turn
kata	cut/turn
tembea	walk
niambie	tell me
kuwa	to be

MAELEZO YA SARUFI - GRAMMAR EXPLANATION

In this lesson, we have used the prepositions:

nyuma ya	-	behind of
mbele ya	-	infront of.
karibu na	-	near by
chini ya	-	under
juu ya	-	on top of
mbali na	-	far from
baina ya	-	between
katikati ya	-	in the middle of

1) These prepositions are equivalent to English to, for, in, anbout, etc. In Kiswahili language, prepositions were originally adverbs and the "ya" itself makes them prepositions. The preposition like "karibu" which is an adverb taken from the Arabic is followed by "NA". So the adverb "Karibu" becomes "karibu na" meaning near by something and "mbali: takes either "Na" or "ya". So "mbali na" will mean far from something. Here are some examples of usage of preposition shown above.

Mwalimu alisimama mbele ya watoto	-	***The teacher stood infront of the children.***
Kikombe kiko chini ya kiti	-	***The cup is under the chair***
Tom yuko karibu na ubao	-	***Tom is near the blackboard.***

2) We have the locative -ko- it is important to note that it is only used in present for example;

M/WA Class:

Niko darasani	-	***I am in class.***
Uko darasani	-	***You are in class.***
Yuko darasani	-	***He/she is in class.***

Plurals:

Tuko nyumbani	-	***We are at home***
Mko nyumbani	-	***You (Plural) are at home.***
Wako nyumbani	-	***We are at home.***

In past and future tenses, the verb "kuwa" in the locative form is used.
For example: In the past tense we get the following:

Hosted for free on livelingua.com

M/WA CLASS
Singular

Jana nilikuwa nyumbani	-	***Yesterday I was at home.***
Jana ulikuwa nyumbani	-	***Yesterday you were at home.***
Jana alikuwa nyumbani	-	***Yesterday he/she was at home.***

Plurals:

Jana tulikuwa nyumbani	-	***Yesterday we were at home.***
Jana mlikuwa nyumbani	-	***Yesterday you (pl) were at home.***
Jana walikuwa nyumbani	-	***They were at home***

FUTURE TENSE "A"
M/WA CLASS

Kesho nitakuwa darasani	-	***Tommorrow I will be in class.***
Kesho utakuwa darasani	-	***Tommorow you will be in class.***
Kesho atakuwa darasani	-	***Tommorrow he/she will be in class***

Plural

Kesho tutakuwa darasani	-	***Tommorrow we will be in class***
Kesho mtakuwa darasani	-	***Tommorrow you (pl) will be in class***
Kesho watakuwa darasani	-	***Tommorrow they will be in class***

MAZOEZI YA SARUFI - GRAMMAR EXERCISES



ZOEZI 1 - EXERCISE 1:

From the words in brackets choose the correct form of the locative -KO- enclitic and complete the sentences below.

1. Mtoto - Chini ya meza (iko, kiko, yuko)
2. Kitabu - Juu ya kiti (yuko, ziko, kiko)
3. Posta - Karibu na Benki (uko, iko, kiko)
4. Mama - Nyumbani (niko, iko, yuko)
5. Watoto - Shuleni (ziko, viko, wako)
6. Mti - karibu na nyumba (uko, iko, liko)
7. Mimi - Darasani (yuko, tuko, niko)
8. Mayai - jikoni (yako, liko, ziko)
9. Nguo - kabatini (viko, ziko, iko).
10. Kalamu - mbali na kitabu (yuko, liko, iko).

ZOEZI 2 - EXERCISE 2

Turn these sentecnes into Kiswahili - Geuza sentensi hizi kwa Kiswahili

1. Yesterday I was at home.
2. Tommorrow I will be a home
3. I was here yesterday morning.
4. The child will be at school.
5. The teachers were in class.

Hosted for free on livelingua.com

6. Students will not be in Malaika.
7. Tommorrow morning I will be in Nairobi.
8. John will not be in class
9. My mother will not be at home tommorrow.

Cultural Note:

In most African countries, directions are usually given using landmarks for example Bridges, rivers or a big tree, building etc. It is rare to hear Kenyans using names of streets, roads and maps when giving directions to a place. Although it varies with particular
Ethnic groups, disctance could be nearer or farther than in actual kilometers. Please
Clarify this with your language trainers and compare differences.

LESSON 16

TOPIC: TRANSPORTATION

COMPTENCY: MAKE BUS AND TRAIN RESERVATION



MAZUNGUMZO I - DIALOGUE I

Kamau:	Habari za leo?	***How are things today?***
Maria:	Nzuri sana.	***Very good.***

Hosted for free on livelingua.com

Kamau:	Ninataka kwenda Mombasa kwa basi, ninaweza kupata tikiti?	***I want to go to Mombasa by Bus. Can I get a ticket?***
Maria:	Unataka kusafiri lini?	***When do you want to travel?***
Kamau:	Ninataka kusafiri Jumamosi.	***I want to travel on Saturday.***
Maria:	Ndio unaweza kupata.	***Yes you can get it.***
Kamau:	Nauli ni pesa ngapi?	***How much is the fare?***
Maria:	Ni shilingi mia tatu.	***It is three hundred shillings.***
Kamau:	Basi litaondoka saa ngapi?	***What time will the Bus leave?***
Maria:	Moja litaondoka saa moja asubuhi na lingine litaondoka saa mbili usiku.	***One will leave at seven in the morning and another one will leave at 8.00 p.m.***
Kamau:	Basi la kwanza hufika Mombasa saa ngapi?	***When does the first Bus arrive Mombasa?***
Maria:	Hufika saa sita mchana.	***It arrives at 12.00 noon.***
Kamau:	Ninataka kusafiri kwa basi la kwanza, kuna nafasi?	***I want to travel by the first Bus, is there space?***
Maria:	Ndio kuna nafasi.	***Yes, there is space?***
Kamau:	Nipe tikiti moja.	***Give me one ticket.***
Maria:	Chukua.	***Take.***
Kamau:	Asante.	***Thank you.***

MAZUNGUM`ZO II - DIALOGUE II

John:	Sasa?	***What's up?***
Awuor:	Fiti sana. Ninaweza kukusaidia?	***Very well. Can I help you?***
John:	Ndio, ninataka kununua tikiti ya kwenda Nairobi.	***I want to buy a ticket to go to Nairobi.***
Awuor:	Ungetaka kusafiri lini?	***When would you like to travel?***
John:	Kesho saa mbili asubuhi.	***Tomorrow at 8.00 a.m.***
Awuor:	Pole bwana, basi la kwanza limejaa lakini kuna nafasi katika basi la pili. Unaweza kusafiri saa nane?	***sorry gentleman, the first bus is full but there is a space in the second bus. Can you travel at 2.00 p.m.?***

Hosted for free on livelingua.com

John:	Ni sawa. Hakuna shida. Ni pesa ngapi?	***It's okey. No problem. How much is it?***
Awuor:	Ni shilingi mia moja. Una mizigo?	***It is one hundred. Do you have luggages?***
John:	Ndio, mfuko mmoja.	***Yes. One bag.***
Awuor:	Basi, jaribu kuwa hapa kesho kabla ya saa nane.	***Then, try to be here tommorrow before 2.00 p.m.***
John:	Sawa sawa, kwaheri tutaonana kesho.	***Okey. Bye, see you tommorrow.***

MSAMIATI - VOCABULARY

NOUNS
M - MI

Umoja - Singular	**Wingi - Plural**	**Kingereza - English**
Mfuko	Mifuko	Bag
Mzigo	Mizigo	Luggage

N CLASS

Umoja - Singular	**Wingi - Plural**	**Kingereza - English**
Tikiti	Tikiti	Ticket
Nauli	Nauli	Fare
Nafasi	Nafasi	Space

VERBS

Ku- pata	to get
Ku- safiri	to travel
Ku-ondoka	to leave
Ku-fika	to arrive
Ku-saidia	to help
Ku-weza	to be able

MAZOEZI - EXERCISE

ZOEZI 1 - EXERCISE

Tafsiri Sentensi sifuatazo - Translate the following sentences:

1. How much is the fare from Nairobi to Mombasa. _____

2. At what time will the first bus leave? _____

Hosted for free on livelingua.com

3. At what time will the bus arrive? _____

4. I want one ticket only. _____

5. Are there seats in this bus? _____

6. I want a front seat? _____

7. Which bus is going to Nairobi _____

8. Who is selling the tickets? _____

ZOEZI II - EXERCISE II

Jifunze Chati iliyo hapa chini na ujibu maswali yafuatayo. Study the Chart below and answer the following questions.

Kusafiri kwa basi - ***Travelling by bus***

Miji Towns	Nauli Fare	Muda wa Kuondoka Time of departure	Muda wa kufika Time of arrival
Nairobi - Mombasa	1300/=	8.00 Asubuhi	12.00 Mchana
Kisumu - Nairobi	400/=	10.00 Asubuhi	2.00 Mchana
Eldoret - Kisumu	300/=	9.00 Jioni	11.00 Jioni
Nairobi - Busia	450/=	12.00 Mchana	5.00 Jioni
Loitokitok - Nairobi	600/=	7.00 Asubuhi	4.00 Jioni
Busia - Kisumu	300/=	7.00 Asubuhi	10.00 Asubuhi

1. Nauli ya basi kutoka Kisumu mpaka Mombasa ni pesa ngapi? _____

2. Basi kutoka Loitokitok mpaka Nairobi hufika saa ngapi? _____

3. Basi kutoka Nairobi mpaka Mombasa huondoka saa ngapi? _____

4. Nauli ya basi kutoka Busia mpaka Kisumu ni pesa ngapi? _____

5. Basi kutoka Eldoret mpaka Kisumu huchukua muda gani? _____

6. Basi kutoka Nairobi mpaka Busia huondoka saa ngapi na hufika saa ngapi? _____

ZOEZI IIII - EXERCISE III

Tafsiri Sentensi hizi - Translate the following sentences.

1. Nauli ya kwenda na kurudi ni pesa ngapi? _____

2. Ningetaka kuketi karibu na dirisha. _____

3. Matatu huchukua muda gani kutoka Nairobi mpaka Kitui? _____

4 Gari la moshi limeondoka _____

Hosted for free on livelingua.com

5. Ninapenda kusafiri usiku _____

6. Basi limejaa hakuna nafasi _____

7. Ninataka kununua tikiti za watu wawili _____

Cultural Note:
"A Matatu is never full" Even if it is full, the touts will always push people to get in. Usually, there is no personal space in public transport.
At times when you go to a Bus Stage the touts will run to you, grab your luggages and take them to their respective vehicles expecting you to follow them. Watch out!

LESSON 17

TOPIC: WEATHER

COMPTENCY: DESCRIBE WEATHER CONDITIONS









Hosted for free on livelingua.com

MAZUNGUMZO - DIALOGUE

Awuor:	Hali ya hewa leo ni nzuri kuliko jana.	***Today the weather is better than yesterday.***
Nzioka:	Ndiyo. Leo ni baridi kidogo. Jana ilikuwa joto kali sana. Lakini kwa kawaida wakati wa kiangazi jua ni kali na kuna joto jingi.	***Yes, Today is a bit cold. Yesterday it was very hot but usually during summer the sun is very hot.***
Awuor:	Kiangazi inaanza lini?	***When does summer begin?***
Nzioka:	Kiangazi ni mwezi wa kwanza mpaka wa tatu. Baada ya kiangazi ni masika.	***Summer is from January to March. After summer is the rainy season.***
Awuor:	Masika huwa vipi?	***How is the rainy season?***
Nzioka:	Masika ni majira ya mvua nyingi sana. Wakati huo watu hupanda mimea mbalimbali. Pia kuna matope mengi sana.	***During the rainy season there is alot of rain. People plant different crops and there is alot of mud.***
Awuor:	Mna majira mangapi?	***How many seasons do you have?***
Nzioka:	Katika Kenya tuna majira manne. Baada ya masika kuna kipupwe ambayo ni mwezi	***In Kenya we have four seasons. after the rainy season there is Winter which is in July and it***

Hosted for free on livelingua.com

	wa saba na huwa na baridi sana.	***is usually very cold.***
Awuor:	Na majira ya nne ni gani?	***And which is the fourth season?***
Nzioka:	Majira ya nne ni ya vuli kutoka mwezi wa kumi hadi kumi na mbili.	***The fourth season fall from October to December.***
Awuor:	Ehe! Hali ya hewa huwa vipi?	***Ehe! How is the weather?***
Nzioka:	Huwa na mvua ndogo na za muda mfupi.	***Usually there is a little rain and for a short time.***
Awuor:	Oh! Asante sana kwa mazungumzo hayo mazuri.	***Oh! Thank you very much for that conversation.***

MSAMIATI - VOCABULARY

NOUNS
N CLASS

Umoja - Singular	**Wingi - Plural**	**Kingereza - English**
Kiangazi	Kiangazi	Summer
Vuli	Vuli	Fall/Autumn
Masika	Masika	Rainy season/spring
KIpupwe	Kipupwe	Winter
Theluji	Theluji	Snow
Jua	Jua	Sun
Majira	Majira	Season
Mvua	Mvua	Rain
Upepo	Upepo	Wind
Vumbi	Vumbi	Dust

M/ MI CLASS

Umoja - Singular	**Wingi - Plural**	**Kingereza - English**
Mmea	Mimea	Plan / crop

MA CLASS

Umoja - Singular	**Wingi - Plural**	**Kingereza - English**
Tope	Matope	Mud
Wingu	Mawingu	Cloud

ADJECTIVES

Kiswahili	**English**
Joto	hot

Hosted for free on livelingua.com

Baridi	cold
Jingi	alot
Kali	very strong

ADVERB

Mbali mbali	different types

VERBS

- Panda	plant, climb
- Nyesha	rain

EXPRESSIONS

Hali ya hewa	air condition (weather)
Hadi	upto / until

MAELEZO YA SARUFI - ***GRAMMAR EXPLANATION ADJECTIVES AND AGREEMENTS***

In this lesson we have used adjectives like - ingi, kali, baridi etc. In Kiswahili adjectives come in three categories as was explained in lesson five i.e. prefix-dependent adjectives beginning with a consonant, prefix-dependent adjectives begining with vowels and prefix independent adjectives. Following are examples of the adjectives under each category.

1. Prefix - dependent adjectives beginning with a consonant.

- zuri	- good, nice, fine beutiful, plesant
- baya	- bad
- bichi	- raw/unripe, uncooked
- bivu	- ripe
- chache	- few
- chafu	- dirty
- changa	- young
- chungu	- bitter, painful
- dogo	- small, little
- fupi	- short
- geni	- new, strange, foreign
- gumu	- hard, difficult
- janja	- cunning, cheeky, clever
- jinga	- studip, ignorant, follish
- kali	- fierce, sharp, strict
- kubwa	- big
- kuu	- great, mighty
- kukuu	- old, tartered
- moja	- one
- nane	- eight
- ngapi	- how many
- nne	- four
- nono	- fat (animals)
- nene	- fat, stout (people)
- nyonge	- weak, feeble, unhealthy
- pana	- wide, broad
- pole	- slow, polite
- pya	- new, fresh
- refu	- long

Hosted for free on livelingua.com

- tamu - sweet, delicious
- tano - five
- tatu - three
- tupu - empty, bare
- tulivu - patient, calm, peaceful
- wili - two
- zee - old
- zima - whole (living beings)
- zito - heavy

II. Prefix dependent adjectives beginning with a vowel

- aminifu - honest, faithful, trustworthy
- ema - good, kind (in character)
- embamba - thin, slender, slim, narrow
- ekundu - red
- epesi - light (in weight) quick, fast
- erevu - clever, cunning (same as janja)
- eupe - white
- eusi - black
- ingi - many, much
- ingine - another, others
- ororo - soft, tender
- ovu - evil

III Prefix - Independent Adjectives - These are usually of origin.

Bora - excellent, better, best, of high quality
Dhaifu - weak
Ghali - Expensive
Haba - a little, few, lacking
Halali - lawful
Huru - free
Hodari - efficient, able, clever, active, strong.
Kamili - Exact, complete
Laini - soft, tender (same as ororo)
Imara - firm, strong
Hafifu - weak, poor, feeble
Kadha wa kadha - several, various
Kila - every, each
gani - what kind of, sort of
Maridadi / Malidadi - beautiful, fancy, adorned
Maskini - poor
Maarufu - famous, well known
Mashuhuri - important, distinguished
Nadhifu - tidy, neat
Safi - clean
Tajiri - wealthy, rich
Shujaa - brave, courageous
Sita - six
Saba - seven
Tisa - nine
Rahisi - cheap, easy

Hosted for free on livelingua.com

Tofauti - different
Mbalimbali - different / various
Kumi - ten

Note:

The adjectival agreements or prefixes are usually the same in form as the noun prefixes. They are used to bring the adjectival stems into agreement with the nouns as in the following examples:

Mtoto mdogo	-	a little child
Watoto wadogo	-	little children
Mti mrefu	-	a tall tree
Miti mirefu	-	tall trees
Kisu kikali	-	a sharp knife
Visu vikali	-	sharp knives
Chumba kichafu	-	a dirty room
Vyumba vichafu	-	dirty rooms



ZOEZI LA KWANZA - EXERCISE ONE

Jibu Maswali haya - ***Answer these questions.***

1. Hali ya hewa iko vipi leo? _____
2. Unapenda hali ya hewa gani na kwa nini? _____
3. Hali ya hewa katika jimbo lako iko vipi sasa? _____
4. Majira ya masika huwa vipi? _____
5. Majira ya kiangazi huanza lini mpaka lini? _____
6. Sasa ni majira gani hapa? _____

ZOEZI LA PILI - EXERCISE TWO

Linganisha hali ya hewa hapa Kenya na hali ya hewa katika America (Compare and contrast the weather in Kenya and in America)

ZOEZI LA TATU - EXERCISE THREE

Andika habari hii kwa kutafsiri maneno yote ya kiingereza katika kiswahili.
(Complete the passage by translating English words into Kiswahili)

Maria ni mtoto **honest** sana. Yeye ni mrefu na **thin,** pia ni **clever**. Juzi jioni Maria alichukua vitabu **two** kimoja **black** and kingine **white**. Kitabu **black** ni **big** kwa hivyo ni **heavy** lakini kitabu **white** ni **light.** Baada ya kuchukua vitabu Maria alikwenda baharini. Alipitia katika barabara **narrow** ambayo ina udongo **red.** Hakuogelea baharini kwa sababu maji yalikuwa na rangi **black**

ZOEZI LA NNE - EXERCISE FOUR

Kutoka kwa jedwali andika vitu ambavyo Baraka huvipenda na ambavyo havipendi:
(From the Chart write the things, which Baraka likes and which he doesn't

Hosted for free on livelingua.com

	-embamba	-ekundu	-eupe	-eusi	-epesi
Rangi		_/	_/	x	
Msichana	_/				_/
Magari		x	_/	x	1
Nguo	_/	_/		x	x
Mvinyo	_/		_/		x
Nyumba		_/		x	
Kitabu		_/	_/	_/	_/
Vitabu		_/	_/	x	_/

Mfano:
Baraka hupenda rangi nyekundu na nyeupe lakini hapendi rangi nyeusi.

1. _____

2. _____

3. _____

4. _____

5. _____

6. _____

ZOEZI LA TANO - EXERCISE FIVE

Tumia adjectives ulizopewa chini kukamilisha sentensi zifuatazo: (***Use the adjectives given below to complete the following sentences)*** bure, ghali, hodari, kamili, kila, laini, rahisi, tele

1. _____ mwaka wakulima hupanda mazao.

2. Sikuinunua redio hii niliipata _____.
iophyuioj

3. Nitakwenda shuleni saa mbili _____.

4. Mkulima _____ alipata mazao mengi.

5. Hapa Kenya matunda ni bei _____ kuliko marekani.

6. Maasai mara hura wanyama _____.

7. Wazee hupenda kula nyama _____.

8. Ni _____ kujifunza Kiswahili.

Cultural Note: There are only two distinct seasons in Kenya namely hot and dry and cold and wet.

Hosted for free on livelingua.com

LESSON 18

TOPIC: CLOTHES AND COLOURS

COMPETENCY: DESCRIBE ARTICLES OF CLOTHING AND COLOURS.

MAZUNGUMZO I - DIALOGUE I

Awuor:	Sasa Jean?	***Hi Jean?***
Jean:	Fiti sana.	***Very fit.***
Awuor:	Una skati maridadi sana. Uliinunua wapi?	***You have a very beautiful Skirt. Where did you buy it?***
Jean:	Niliinunua sokoni kwa mtumba	***I bought it at the market, it's a used one (second hand)***
Awuor:	Ninapenda rangi yake.	***I like its colours.***
Jean:	Mimi pia. Ninapenda buluu na waridi.	***me too, I like blue & pink***

Hosted for free on livelingua.com

Awuor:	Uliinunua pesa ngapi?	***How much did you buy it?***
Jean:	Shilingi mia moja na hamsini tu!	***A hundred and fifty shillings only.***
Awuor:	Mmh! Ni bei rahisi sana. Utanipeleka hapo? Ningependa kununua pia.	***Very cheap.*** ***Will you take me there?*** ***I would like to buy .***
Jean:	Sawa nitakupeleka Jumatano ijayo.	***I will take you there next Wednesday.***

MSAMIATI - VOCABULARY

KI/VI - CLASS

Kiatu	Viatu	Shoes
Kipuli	Vipuli	Ear rings
Kitambaa	Vitambaa	Head Scarf
Kikoi	Vikoi	A piece of cloth used by men
Kinyasa	Vinyasa	shorts

M/MI CLASS

Umoja - Singular	**Wingi - Plural**	**Kingereza - English**
Mshipi	Mishipi	Belts
Mtumba	Mitumba	Used clothes

N CLASS

Hosted for free on livelingua.com

Soksi	Soksi	Socks
Blausi	Blausi	Blouse
Skati	Skati	skirt
Shati	Shati	Shirt
Kofia	Kofia	Hat, Cap
Tai	Tai	Tie
Leso/Kanga	Leso/Kanga	Piece of cloth used by women
Suti	Suti	Suit
Sweta	Sweta	Sweater
Koti	Koti	Coat
Jaketi	Jaketi	Jacket
Kamisi	Kamisi	Slip
Chupi	Chupi	Underwear
Sindilia	Sindilia	Brazier
Nguo	Nguo	Dress/Cloth
Fulana	Fulana	Vest
Kanzu	Kanzu	Gown worn by Muslim men
Patipati	Patipati	Slippers
Buibui	Buibui	Black long dress worn by Muslim women
Pete	Pete	Ring
Saa	Saa	Watch
Bangili	Bangili	Bangle(s)
Miwani	Miwani	Spectacles

VERBS

Kuvaa - to wear

Adjectives

-eupe	White
-eusi	Black
-ekundu	Red
Machungwa	Orange
Manjano	Yellow
Kijani kibichi	Green
Buluu	Blue
Waridi	Pink
Zambarao	Purple
Kahawa / kahawia	Brown
Kijivu	Grey
Samawati	Light Blue
Dhahabu	Gold
Fedha	Silver
Almasi	Diamond
Madoadoa	Spots
Mistari	Stripe

GRAMMAR EXPLANATION - MAELEZO YA SARUFI

Hosted for free on livelingua.com

Apart from -eusi, -eupe, -ekundu which are prefix dependent. Other colours are Underpendent, for example:

Mtu mweusi	-	Watu weusi
Kitabu chekundu	-	Vitabu vyekundu
Kalamu nyeusi	-	Kalamu nyeusi.

Nguo ya kijani kibichi
Shati la manjano.
However, when modifying nouns, connectors are used -ya (of) to which appropriate prefixes are attached examples.
Hence:

Nguo ya kijani kibichi	-	Nguo za kijani kibichi.
Shati la manjano	-	Mashati ya manjano.
Kiatu cha waridi	-	Viatu vya waridi.


However, undependent colours are frequently used as adjectival phrases, **for examples.**

Nguo ya rangi ya buluu	-	**A blue cloth / pieces of clothing**
Shati la rangi ya manjano		**A yellow shirt.**
Kiatu cha waridi	-	**A yellow shirt.**
Skati ya rangi ya zambarau		**A purple skirt.**

ZOEZI LA KWANZA - EXERCISE ONE

Jaza nafasi hizi - Complete ***the following sentences using the correct noun agreement***
Example:
Mwalimu wangu amevaa viatu ____kundu. -Mwalimu wangu amevaa viatu vyekundu.

1. Paka wako ni _____eupe si _____eusi.
2. Kijana huyu amevaa viatu ____eusi.
3. Kuna watu ____ eusi wengi katika Amerika.
4. Kwa nini watu wanaoishi jangwani huvaa nguo ____eupe?
5. Koti la Ezekiel ni _____ ekundu
6. Mwalimu wake amevaa shati _____ rangi _____kijani kibichi.
7. Hana mashati ____eupe lakini nina shati _____rangi ____ kijivu.



Cultural Note:

- People dress for others. You dress according to who you are going to meet i.e. special occasions like graduation, parties, ceremonies, church etc.

Hosted for free on livelingua.com

- All women are required to wear slips especially when wearing transparent (see me through) dresses.

- Apart from the three dependent colours (-eupe -eusi & -ekundu) all other colours are named after natural things. Examples.

Sharti la kijivu.	-	An ash *coloured shirt*	*- a grey shirt*
Skati ya kijani kibichi	-	*A skirt of fresh leaf*	*- a green skirt.*
Koti la kahauria	-	*a coat of coffee*	*- a brown coat.*
Pete ya Dhahabu	-	*a ring of Gold*	*- a Golden ring.*

LESSON 19

Hosted for free on livelingua.com

TOPIC: TRANSPORTATION

COMPETENCY: BOOKING A ROOM

DIALOGUE 1 - MAZUNGUMZO I

Scott:	Hujambo bwana Karani?	***Halo Mister Clerk?***
Clerk:	Sijambo. U hali gani?	***Hallo in which state are you?***
Scott:	Salama tu Ninaweza kupata chumba hapa?.	***Just fine. Can I get a room here?***
Clerk:	Ndio, ungetaka chumba cha aina gani?	***Yes what kind of room would you like?***
Scott:	Chumba cha watu wawili chenye choo na bafu ndani. Pesa ngapi?	***A double room with a toilet and Bathroom inside. How much is it?***
Clerk:	Ni shilingi mia nane kwa usiku mmoja. Utakaa kwa muda gani?	***Eight hundred per night For how long will you stay.***
Scott:	Kwa usiku mmoja tu. Chukua pesa na unipe ufunguo.	***Just one night. Here is the money give me the key.***
Clerk:	Sawa. Utatumia chumba nambari tisa.	***Okay, you'll use room number nine.***
Scott:	Utanipa risiti?	***Will you give me a receipt?***
Clerk:	Ndio kesho asubuhi.	***Yes, tommorrow morning.***
Scott:	Haya asante.	***Okay, Thank you.***

DIALOGUE 2 - MAZUNGUMZO YA PILI

Chris:	Vipi bwana?	***How is it Dude?***
Bosco:	Poa.	***Cool.***
Chris:	Una chumba hapa?.	***Do you have a room?***
Bosco:	La, vyote vimejaa	***No they are all full. (fully booked)***
Chris:	Ni hoteli nyingine gani ninaweza Kwenda?	***Which other good hotel can I go?***
Bosco:	Nenda Parkside, karibu na Jivanjee Garden.	***Go to Parkside near Jivanjee Garden.***

Hosted for free on livelingua.com

Chris:	Wana maji moto?	***Do they have hot showers?***
Bosco:	Ndio. Hata na neti za mbu. Utakuwa na usiku poa sana hapo.	***Yes, even Mosquito nets. You will have a very calm night there.***
Chris:	Wanauza vinywaji?	***Do they sell drinks.***
Bosco	Naam, vya kila aina na chakula pia.	***Yes, of all kinds and food too.***
Chris:	Asante rafiki. Tutaonana.	***Thank you. See you.***
Bosco:	Kwaheri	***Bye bye.***

DIALOGUE 3 - MAZUNGUMZO YA TATU

Karani:	Karibu bwana. Habari gani?	***Welcome how are you?***
Mgeni:	Safi.	***Clean (fine)***
Karani:	Ninaweza kukusaidia?	***Can I help you?***
Mgeni:	Ndio, ninahitaji chumba cha mtu mmoja chenye choo na bafu ndani. Inawezekana?	***Yes, I need a self contained room. Is it possible?***
Karani:	Ndio, unakitaka kwa muda gani?	***Yes for how long do you need it?***
Mgeni:	Kwa wiki moja. Ni pesa ngapi?	***For a week. How much is it?***
Karani:	Ni elfu moja kwa usiku mmoja	***One thousand per night.***
Mgeni:	Sawa. Hizi ni pesa za wiki moja.	***Okay. This is money for one week.***
Karani:	Asante. Nitakupa chumba nambari ishirini.	***I'll give you room number Twenty.***
Mgeni:	Ninaweza kupata chakula hapa?	***Can I get food here?***
Karani:	Ndio, kuna kengele ndani ya chumba chako. Finya kisha weita atakuja kukuhudumia. Chakula chako kitaletwa kwenye chumba chako.	***Yes, there's a bell inside your room. Press it and the weita will come to serve you. Your food will be brought into your room.***
Mgeni:	Asante bwana. ***Okay.***	***Thank you sir.***Karani: Sawa sawa.

MSAMIATI - VOCABULARY

M/WA

Hosted for free on livelingua.com

Mgeni	Wageni	Guest, visitor(s)
Karani	Makarani	Clerk(s)
Mtalii	Watalii	Tourist(s)
Chumba	Vyumba	Room(s)

N CLASS

Risiti	Risiti	Receipt
Muda	Muda	Period
Kengele	Kengele	Bell(s)
Neti ya Mbu	Neti ya Mbu	Mosquito net
Bafu	Bafu	Bathroom(s)
Ghorofa	Ghorofa	Storey(s)
Lifti	Lifti	Lift, elevator

U CLASS

Ufunguo	Funguo	Key(s)
Usiku	Usiku	Night(s

VERBS

Kupa	-	Give
- pendelea	-	Prefer
- saidia	-	Help
kuwa na	-	have, be with
- uza	-	sell
- pokea	-	receive
- pata	-	get
- kodisha	-	rent

MAELEZO YA SARUFI - GRAMMA EXPLANTION

In this lesson, the main grammar aspect that needs to be explained is -ENYE, as an Adjectival phrase meaning “Having”, Possessing, or ’ “with” - Enye is a prefix dependent stem denoting “Being with” or “Having”, it is frequently used.

Examples;

Mtu mwenye afya	-	**a person having health**	**(healthy person)**
Chumba chenye baridi-		**a room having coldness**	**(a cold room)**
Chjungwa lenye maji	-	**an orange having water**	**(a juicy orange)**

The prefix that you place before this adjectival phrase depends on the noun class, However, when SUFFIX -WE is added to -ENYE the meaning changes to:

i) Self or selves (distinctness)

e.g.a) Nitaenda mwenyewe - **I will go myself**

b) Gari lenyewe - **The vehicle itself.**

ii) Owner e.g.


Hosted for free on livelingua.com

a) Mwenyewe hayupo - **The owner is not there.**
b) Wenyewe wamesafiri - **The owners have travelled.**

Note: In M/WA Class, the noun, may be omitted yet both the speaker and the listener will understand each other

ZOEZI 1 - EXERCISE 1

Jibu Maswali haya - Anwer These Questions:



1. Hapa Kenya umekaa katika hoteli gani?
2. Ulikaa Kwa muda gani?
3. Ulikaa peke yako?
4. Ulikuwa unakula katika hoteli hiyo?
5. Ulilipa pesa ngapi kwa siku?
6. Ulikaa katika chumba cha aina gani?
7. Hoteli hiyo ulikuwa na ghorofa? Ngapi?
8. Umewahi kutumia lifti kupanda ghorofa?
9. Katika Kenya vyumba vya kukodisha ni kama vya Amerika?

ZOEZI I - EXERCISE I

Tafsiri Sentensi hizi - Translate these sentences:

1.I want a house, which has a bathroom and a toilet.

2.This room is cold, I don't like it.

3.I don't like salty food.

4.Buffaloes are animals with long horns.

5.I don't like staying in a very dark room.

6.The owner of that house died last year.

7.That healthy old man came yesterday.

ZOEZI III - EXERCISE III

Hosted for free on livelingua.com

Tumia maneno haya katika sentensi zako mwenyewe. Use these phrases to create your own sentences.

1. Kitabu chenye _____
2. Kalamu yenye _____
3. Duka lenye _____
4. Kijana mwenye _____
5. Mahali penye _____
6. Ulimwengu wenye _____
7. Mtoto mwenye _____
8. Chungwa lenye _____
9. Ukuta wenye _____

ZOEZI IV - EXERCISE IV

Andika sentensi hizi Kwa wingi - Write these sentences in plural

1. Mwanafunzi mwenyewe ni mtukutu sana.
2. Kikombe chenyewe kilivunjika jana.
3. Nyumba yenyewe imejaa wageni.
4. Tunda lenyewe limeoza.
5. Mkate wenyewe umeungua.
6. Mti wenyewe umekauka.
7. Tanki lenyewe limejaa maji.
8. Msichana mwenyewe ni mrembo sana.

Cultural Note:

- *In some Kenyan hotels, you might be told that there is hot water for showers but in the next morning there won't be any, and you'll be given excuses.*

Hosted for free on livelingua.com

- *Sleeping in lodging by opposite sex, people is associated with prostitution. So when you tell your friends that you slept in a lodging they might mistake you for a loose woman or man. Instead you call it a hotel.*

- *When you go to book a room with someone of your opposite sex, the receptionist might expect you to share a room.*

Hosted for free on livelingua.com

TECHNICAL COMPETENCIES

Hosted for free on livelingua.com

AGROFORESTRY COMPETENCY

KUJIJULISHA - INTRODUCTION

MAZUNGUMZO A - DIALOGUE A	
PCV : - Hujambo. **Mkulima:** - Sijambo**.** **PCV** : - Habari ya kazi. **Mkulima** : - Nzuri na wewe. **PCV** : - Nzuri pia. **PCV** : - Jina langu ni Michi, ninatoka nchi ya Amerika, ninafanya kazi na Peace Corps hapa Kenya. **Mkulima**: - Peace Corps ni nini? **PCV** : - Peace Corps ni shirika kutoka Amerika na wanafanya kazi katika nchi tofauti tofauti. **Mkulima**:Na wanafanya kazi gani? **PCV** : - Wanafanya kazi kama kufundisha katika shule, kazi ya maji, msitu, na kuwashauri wafanyi biashara ndogo ndogo.	**PCV:** Hallo **Farmer:** Fine **PCV:** How is work **Farmer**: Fine and you **PCVs:** Fine also **PCV**: My name is Michi, I come from America, I work with Peace Corps here in Kenya. **Farmer:** What is Peace Corps? **PCV:** Peace Corps is an organization from America and has volunteers who work in different countries. **Farmer:** And which work do they do? **PCV:** They do work like teaching in schools, Water and Health, Forestry and Small Business advisory.

Hosted for free on livelingua.com

MAZUNGUMZO B - DIALOGUE B **PCV :** Habari yako. **Mkulima**: Nzuri. **PCV :** Mimi ni mwana Peace Corps ninasaidia kuwapa mawaidha wakulima. **Mkulima:** Unafanya kazi na watu gani? **PCV :** Ninafanya kazi na watu wa misitu.	 **PCV**: How are you **Farmer:** Fine **PCV:** I am a Peace Corps Volunteer helping in giving advice to farmers **Farmer:**, You work with which people? **PCV:** I work with forestry people

Msamiati	**Plural**	**English**
Shirika	Mashirika	Organization
Msitu	Misitu	Forest
Mkulima	Wakulima	Farmer
Kupanda	Kupanda	To grow/plant
Mti	Miti	Tree
Kusaidia	Kusaidia	To help
Mawaidha	Mawaidha	Ideas
Shamba	Mashamba	Farm
Kilimo mseto	Kilimo mseto	Agro-forestry
Kushauri	Kushauri	Advice

ZOEZI LA KWANZA - EXERCISE ONE

Andika kwa Kiswahili - write in Swahili:

1) I am a PCV
2) He/She is an Agroforester.
3) This is a farmer.
4) I am helping farmers.
5) He is planting trees in his farm.
6) I give farmers ideas on Agro-forestry.
7) Which organization do you work for.
8) Peace Corps Volunteers work as Agro-foresters, Water Technicians.

Hosted for free on livelingua.com

TOPIC : KILIMO MSETO
COMPETENCY : IMPORTANCE OF TREES IN THE FARM:

Hosted for free on livelingua.com

UMUHIMU WA MITI SHAMBANI	
Mama Mwikali ni mkulima katika sehemu ya katumani. Ana miti tofauti ambayo amepanda pamoja na mimea ya chakula. Mimea hii ya chakula ni kama mahindi, maharagwe, miti ya, matunda, na miti aina tofauti.	Mama Mwikali is a farmer in Katumani. She has different trees that she has planted together with food crops. These food crops are like maize, beans, fruit trees and different types of trees.
Miti humpa kuni, mbao za kujenga nyumba na chakula cha mifugo kwa kutumia majani ya miti. Watu na mifugo hupumzika chini ya kivuli cha miti wakati wa jua kali. Mingine huzuia upepo na mingine ni ua la shamba lake.	Trees give her firewood, timber and fodder from leaves. People and animals rest in the shade from trees when it is hot. Other trees prevent wind while others are live fence.
Wakati wa mvua miti huzuia mmomonyoko wa udongo kwa kushikilia udongo kwa mizizi katika shamba la mama Mwikali. Mizizi ya miti huongeza rutuba udongoni na pia majani yaangukayo, jambo, ambalo huongeza mazao shambani. Mama Mwikali huuza mazao yake sokoni kama mahindi matunda na anapata pesa nyingi.	During rain season, roots hold soil and thus prevent soil erosion in Mama Mwikali's farm. Roots add fertility to the soil and also leaves which fall, a matter which increase food production. Mama Mwikali sells her produce in the market like maize fruits and she gets a lot of money.

Hosted for free on livelingua.com

JINSI YA KUPANDA MITI. **HOW TO PLANT TREES.** Miti tofauti inaweza kupandwa pahali tofauti shambani. Unaweza kupanda miti kati ya mimea; mipakani ya shamba, kama ua au kuzuia upepo, pia kama ua la boma, kando ya mto au pahali pa mawe mengi. Miti ambayo hupandwa kati ya mimea ni ile ambayo mizizi yake ni michache na huelekea chini ili isitumie maji na chakula cha mimea. Aina hii ya miti haina kivuli kizito lakini huongeza rotuba udongoni. Miti ambayo hupandwa mpakani ni mirefu na yenye nguvu za kuzuia upepo mkali. Miti ambayo inafaa kupandwa kama ua la boma ni miti ina miiba kwa usalama na ambayo inaweza kukua karibu karibu. Ni muhimu kujua jinsi ya kutunza miti hii. Miti ambayo imepandwa pamoja na mimea hupunguzwa matawi ili kuipa mimea nafasi ya kukua na inapofika kiwango fulani hukatwa kabisa ili ikue upya. Ile miti ambayo iko kwenye mipaka ya shamba hupunguzwa matawi ya chini na kuachwa iwe mirefu ili iweze kuzuia upepo	Different trees can be planted at different places in the farm. You can plant among crops, boundaries,fence or to prevent wind, also as home stead fence banks of rivers or stoney places. Trees that are planted among crops are those wwith tap roots so as not to complete for water and food with crops. These types of trees do not hve big shades but add fertility to the soil. Trees which are planted along bounderies are tall and strong to prevent strong winds. Trees suitable as live or homestad fence are trees having thorns for security and which can groww closely. It is important to know how to care for these trees. Trees that are planted among crops should be trimmed to give chance to the growing crops and at certain level they are completely cut to enable them grow a fresh. The lower branches of trees growwn along the boundries are usually pruned and left to be long so as to prevent wind.

MSAMIATI - VOCABULARY:

Kiswahili (Singular)	**Plural**	**English**
Mjitoleaji	Wajitoleaji	Volunteer
Mkulima	Wakulima	Farmers
Kilimo	-	Agriculture
Kilimo Mseto	-	Agroforestry
Kukuza (V)		To grow
Kufuga (V)	-	To rear
Mfugo	Mifugo	Livestock
Kupanda (V)	-	To plant
Mmea	Mimea	Plants
Shamba	Mashamba	Farm
Mnyama	Wanyama	Animals
Umuhimu (abstract)	Umuhimu	Importance
Mzizi	Mizizi	Roots
Sehemu	Sehemu	Area/Part
Kujenga (V)	-	To build

Hosted for free on livelingua.com

Rotuba	Rotuba	Fertility
Udongo	Udongo	Soil
Zao	Mazao	Produce (N)
Ua	-	Fence
Kuzuia (V)		To prevent
Mmomonyoko	Mmomonyoko	Erosion
Kushikilia (V)	-	To hold
Kuni	Kuni	Firewood
Mbao	Mbao	Timber
Boma	Maboma	Homestead
Nafasi	Nafasi	Space
Mpaka	Mipaka	Boundry/boarder
Upepo	Upepo	Wind
Mwiba	Miiba	Thorns
Kiwango	Viwango	Level / extent
Tawi	Matawi	Branches

UFAHAMU - COMPREHENSION I

1) Mama Mwikali anaishi wapi?
2) Yeye hupanda nini katika shamba lake?
3) Miti humpa faida gani?
4) Wakati wa mvua miti huzuia nini?
5) Mama Mwikali huuza mazao yake wapi?
6) Miti hupandwa wapi shambani?
7) Ni miti gani hupandwa katikati ya mimea?
8) Ni miti gani hupandwa mipakani?
9) Kwa nini miti hupandwa uani?
10) Miti inayopandwa uani na ile inayopandwa mipakani hutuzwa vipi?
11) Mmomonyoko wa udongo ni nini?
12) Kilimo mseto ni nini?

Hosted for free on livelingua.com

TOPIC: **TREE NURSERY - (NASARI YA MICHE)**

COMP: **TEACH FARMERS WHEN, WHY WHERE AND HOW TO CONSTRUCT A TREE NURSERY.**
(KUFUNDISHA WAKULIMA LINI, KWANINI, WAPI NA JINSI YA KUJENGA NASARI YA MITI.

MAZUNGUMZO YA KWANZA - (DIALOGUE ONE)

PCV :Habari zenu?	**PCV:** How are you (plural)
Wakulima:Nzuri sana.	**Farmer**: Very fine
PCV: Tulipokuja hapa Kihoto na Afisa wa misitu, mlitueleza juu ya shida zenu na leo nimekuja ilikujaribu kuwasaidia. Je mnajua nasari ya miche?	**PCV:** When we came here to Kihoto with the Forest Officer, you told us about your problems and today I have come so as to try and help you. Well, do you know a tree nursery?
Mkulima: Ndiyo kwa mfano nasari ya mboga.	Farmer: Yes for example vegetable nursery.
PCV : Asante sana. Sasa ningependa moja wenu atuambie mahitaji ya nasari.	PCV: Thank you very much, now I would like one of you to tell us on the needs of a tree nursery.
Mkulima:Ni bora kutayarisha nasari karibu na maji na kivulini.	**Farmer:** It's better to prepare a tree nursery next to water and shade.
PCV: Asante sana bwana. Pia tunahitaji pahali ambapo:-	**PCV:** Thank you sir, also we need a place where:
a) Hapana maji mengi b) Pahali ambapo wanyama, watu na mvua nyingi haiwezi kuharibu.	a) Doesn't have a lot of water. b) Place where animals, people and a lot of rain can not destroy.
Wakulima: Asante sana bwana sasa tumefahamu.	**Farmer**: Thank you very much sir, now we have understood.
PCV :Ikiwa ninatayarisha nasari ninahitaji nini?	**PCV:** If I am preparing a tree nursery what do I need?
Mkulima: Tunahitaji; udongo, panga, mbolea, jembe na mbegu.	**Farmer:** We need soil, panga, manure, hoe and seeds.
PCV :Pia mnahitaji vijiti, kivuli, migomba, mbao, magogo matofali au mawe.	**PCV:** Also you need, sticks, shade banana stems timber, logs and bricks or stones.
Wakulima: Sasa tumefahamu. Kesho tutaleta vitu vyote, halafu tutatayarisha nasari.	**Farmer:** Now we have understood. Tomorrow we will bring everything, then we will prepare a nursery.
PCV :Haya tutaonana kwaherini.	**PCV**: Okay we will see each other bye.
Wakulima: Kwa heri asante sana.	**Farmer:** Bye thank you very much.

Hosted for free on livelingua.com

MAZUNGUMZO YA PILI (SECOND DIALOGUE)

JINSI YA KUTAYARISHA NASARI (HOW TO PREPARE A NURSERY)

PCV :Hamjambo wakulima.	**PCV:** Hallo farmers
Wakulima: Hatujambo bwana habari yako.	**Farmers:** We are fine sir, how are you?
PCV :Njema, mmeleta vitu vya kutayarisha nasari?	**PCV:** Fine, have you brought things to prepare a nursery?
Wakulima:Ndiyo tumeleta.	**Farmers**: Yes we have brought.
PCV :Asanteni sana. Ikiwa unataka kutayarisha nasari unafanya nini?	**PCV:** Thank you very much. If you want to prepare a nursery, what do you do?
Mkulima:Kwanza, unahitaji kufyeka, na kuchimba mahali ambapo unataka kutayarisha nasari. Halafu tandaza udongo kwa kutoa takataka.	**Farmer:** First, you need to slash and dig a place that you want to prepare a nursery, then flatten the soil by removing rubbish.
PCV: Baadaye utafanya nini?	**PCV:** Later what will you do?
M**kulima II:** Utachukua vijiti vya upana wa inchi saba na viwili vya urefu wa futi moja na nusu na vingine viwili vya urefu wa futi tatu vya kushikilia udongo.	**Farmer II:** You will take sticks of seven inches wide and two sticks of one and a half feet long and another two sticks of three feet long for holding the soil.
PCV :Oh, vizuri kabisa. Na utafanya nini na vijiti?	**PCV:** Oh, very good. And what will you do with the sticks?
Mkulima III: Utatumia vijiti kutengeneza sanduku, pigilia vijiti vidogo kwa kila kona kushikanisha sanduku.	F**armer:** You will use sticks to prepare a box, pitch small sticks in every corner to hold together the box.
PCV : Pia unahitaji kuchanganya karai mbili za udongo ambao unarotuba na karai moja ya mbolea. Halafu weka udongo ambao umechanganya na mbolea ndani ya sanduku na tandaza. Sasa nasari ni tayari kwa kupanda mbegu zako.	**PCV:** Also you need to mix two basins of fertile soil and one basin of manure. Then put the soil that you have mixed in the box and flatten. Now the nursery is ready for planting your seeds.
Mkulima IV: Unatayarisha nasari wakati gani?	**Farmer IV:** When do you prepare a nursery?
PCV : Hilo ni swali muhimu sana!. Hakikisha umetayarisha nasari yako miezi miwili kabla ya mvua kuanza.	**PCV:** That is a very important question. Make sure you have prepared your nursery two months before the rain starts.

Hosted for free on livelingua.com

SOMA KWA SAUTI (READ ALOUD)

Miche ya miti.
Changanya udongo na mbolea.
Pigilia kijiti.
Pigilia mgomba.
Pigilia gogo.
Chini ya kivuli.
Ukosefu wa maji.
Ukosefu wa miche.
Ukosefu wa mbegu.
Kutayarisha nasari.
Kutayarisha mbegu.
Kutandaza udongo.
Kutengeneza sanduku.
Chimba mahali.
Kushikanisha sanduku.

VOCABULARIES:

Msamiati		**Misamiati**	**Vocabulary**
Mkaazi	(n)	Wakaazi	Residents
Ukosefu	(n)	Ukosefu	Lack
Mbao	(n)	Mbao	Wood
Mkutano	(n)	Mikutano	Meeting
Miche	(n)	Miche	Seedling
Msitu	(n)	Misitu	Forest
Nasari	(n)	Nasari	Nursery
Kulowa	(v)	Kulowa	To be wet
Kifaa	(n)	vifaa	Tool
Panga	n)	Panga	Panga
Mbegu	(n)	Jembe	Hoe
Mgomba	(n)	Migomba	Banana stem
Jiwe	(n)	Mawe	Stone
Kujadili	(v)	Kujadili	To discuss
Kuni	(n)	Kuni	Firewood
Kujenga	(v)	Kujenga	To build
Kupanda	(v)	Kupanda	To climb
Mti	(n)	Miti	Trees
Kutatua	(v)	Kutatua	To solve
Hitaji	(n)	Hitaji	To need
Mnyama	(n)	Wanyama	Animal
Udongo	(n)	Udongo	Mud
Kutayarisha	(v)	Kutayarisha	To prepare
Kutandaza	(v)	Kutandaza	To flatten

ZOEZI LA KWANZA - EXERCISE ONE:

Hosted for free on livelingua.com

MKUTANO WA WATU WA KIJIJI CHA KIHOTO:

Watu wa Kijiji cha Kihoto walikutana ili kuzungumza juu ya shida zao. Shida hizo zilikuwa; ukosefu wa kuni na mbao za kujenga. Mwenyekiti wa mkutano alikuwa mzee wa kijiji, waliona kwamba, bei ya mbao imekuwa ghali, na pia miche ya miti ambayo walipata kutoka kwa serikali haikutosha na pia ilikuwa ya aina moja. Baadaye waliamua kualika afisa wa misitu. Afisa wa misitu alifika pamoja na mwana Peace Corp.

Afisa wa misitu alimjulisha mwana Peace Corp kwa watu wa kijiji cha Kihoto. Mwana Peace Corp alipanga siku ya kukutana na wana kijiji wa Kihoto.

MASWALI - QUESTIONS:

1) Watu wa Kijiji cha Kihoto walikuwa na shida gani?
2) Nani alikuwa kiongozi wa mkutano?
3) Afisa wa misitu aliwasaidia vipi?
4) Mwana Peace Corp alipanga kukutana na wana kijiji wa Kihoto, unafikiri kwa nini?

JIBU MASWALI HAYA (ANSWER THESE QUESTIONS)

1) Unahitaji kutayarisha nasari ya miche wapi?
2) Unahitaji nini ili kutayarisha nasari ya miche?
3) Ikiwa unataka kutayarisha nasari, kwanza utafanya nini?
4) Baada ya kutandaza udongo utafanya nini?
5) Utatumia vijiti vipi?
6) Unachanganya vipi mbolea na udongo na kisha utafanya nini?

Hosted for free on livelingua.com

KUTAYARISHA MBEGU - SEED TREATMENT:

MAZUNGUMZO - DIALOGUE

Tom: Hujambo.	**Tom:** Hallo
Mkulima:Sijambo, habari gani?	**Farmer:** Fine, how are you?
Tom :Njema labda yako.	Tom: Fine maybe you?
Mkulima: Njema tunaendelea na kazi tu.	**Farmer:** Fine we are continuing only with work.
Mkulima: Nilipanda mbegu zangu lakini naona hazikuota zote. Unafikiri kwa nini?	**Farmer:** I planted my seeds but all didn't germinate. Why do you think so?
Tom : Labda hukutayarisha mbegu zako vizuri.	**Tom:** Maybe you didn't prepare your seeds well.
Mkulima: Ninahitaji kutayarisha kabla ya kupanda?	**Farmer:** Do I need to prepare before planting?
Tom : Ndiyo ni muhimu sana kutayarisha mbegu zako kabla ya kupanda.	**Tom:** Yes it is very important to prepare your seeds before planting.
Mkulima: Ni muhimu kwa nini?	**Farmer:** Why is it important?
Tom : Kwa sababu kuna mbegu tofafuti. Megu zingine zina maganda magumu na haziwezi kumeza maji kwa upesi.	**Tom:** Because there are different seeds, other seeds have hard husks and cannot absorb water easily.
Mkulima: Ehe.	**Farmer:** Ehe.
Tom : Mbegu kama Tamarindus indica (mkwaju),huwekwa ndani ya maji moto na kulala usiku mzima.	Tom: Seeds like Tamarindus Indica are put in hot water and stay over night.
Mkulima: Na hizi zinaitwa Acacia Mearnsii (Black Wattle) ambazo nilinunua wiki iliyopita?	**Farmer:** What of these called Acacia Mearnsii (black wattle) that I bought last week?
Tom : Hizo hufunikwa kwa udongo mwepesei na majani katika nasari halafu majani huchomwa moto.	**Tom:** Those are covered with light soil and grass in the nursery and burnt.
